# YALIYONIKUTA TANGA

Mohammed Hammie Rajab

**Dar. Gen. Publishing House**
**Dar es Salaam**
**Tanzania**

Kimechapishwa na:
Dar General Publishing House,
Dar es Salaam, Tanzania
muddybtz@gmail.com
+255 713538427

© Mohammed Hammie Rajab, *2020*

**Simu**: +255 625 634 902, +255 719 000 010
E-mail: ankomo25@yahoo.com

Jalada: Hassan Dambaya / Kindo Arts

Mhariri: Hussein Wamaywa
Michoro: Marco Tibasima
Msanifu kurasa: John Wise / Muddyb Mwanaharakati

**Chapa ya kwanza, 2020**

**ISBN**: **978-9976-88-057-1**

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kuiga, kukitafsiri, kukipiga chapa kitabu hiki kwa namna yoyote kwa ajili ya biashara bila idhini au makubaliano kutoka kwa mtunzi na mwandishi wa kitabu hiki.

**TUNU**
**Kwa marehemu baba yangu:**

## Hammie Rajab



Ulitimiza wajibu wako baba, hazina ya maandishi uliyoiacha haiwafai Watanzania pekee bali na dunia kwa ujumla. Upumzike kwa amani sasa kwa kuwa mwanao nimeanza kufuata nyayo zako baba, kuutimiza kwa vitendo usemi usemao mtoto wa nyoka ni nyoka. Nimeanza kufanya kitu ulichokipenda sana, ulipoteza muda wako, nguvu pamoja na akili nyingi kuandika riwaya zilizowavutia wengi. Mpaka leo pamoja na kuwa haupo, lakini bado watu wengi wanakufurahia na kuzisemea kazi zako. Kitu kimoja tu ujue baba, tulikupenda, tunakupenda na tutaendelea kukupenda. Allah akupe kauli thabiti baba. Amina!

## Kanusho

Simulizi hii ni ya kubuni. Haihusiani na tukio lolote la kufanana. Iwapo kuna mfanano wa matukio ya aina yoyote basi haikuwa dhamira ya mtunzi na mwandishi.

## UTANGULIZI

Wakati Musa anaianza safari yake ya kutoka Arusha kwenda Tanga, aliamini yale yote aliyoambiwa na rafiki yake Maliki kuhusiana na uzuri wa mji huo pamoja na watu wake.

Mabinti wa kitanga na ufundi wao wa mapishi, ulaini wa lugha yao, ujuzi wa mapenzi na uwiano asilia kati yao na neno PENZI.

Simulizi za kubebwa mgongoni huku ukiandaliwa maji vuguvugu ya kuoga yenye harufu nzuri ya hiliki, zilijirudia mara kwa mara mawazoni mwake kadiri anavyolisogelea jiji hili la bandari ya Kaskazini mwa Tanzania. Hii ni fursa ya kuyashuhudia.

Akiwa Tanga Musa aliyejaa na matamanio ya kupata raha za mapenzi ya ki-Tanga anakutana na Zuhra katika klabu moja maarufu ya usiku ya Lacasa Chica.

Matumaini ya Musa yanapotea ghafla! Maskini, hakujua kama alikuwa katika mtego mkubwa uliogubikwa na dhana potofu zilizopelekea ajutie yanayomkuta baada kukutana na binti huyo mwenye asili ya kiarabu.


Fuatilia kisa hiki kinachosimuliwa na Mohammed Hammie Rajab, mtoto wa aliyekuwa gwiji la uandishi Tanzania marehemu Hammie Rajab ili ujue ni yapi YALIMKUTA Musa akiwa Tanga.

# SURA YA KWANZA

… Kwa mujibu wa yule dereva teksi, tulikuwa tayari tumekwishafika katika eneo alilolitaja kuwa ni *four ways*, moja kati ya eneo maarufu linalokutanisha barabara nne mahali pamoja hapa Tanga mjini. Hakukuwa na purukushani ya magari kwa kuwa ilikuwa ni usiku.

Pamoja na kwamba kulikuwa na giza hafifu lakini niliweza kuona baadhi ya majengo yaliyokuwa pembezoni mwa barabara hiyo kutokana na taa za gari zilizokuwa zikimulika wakati tunaikaribia kona ya kuingia upande wa kushoto, kitendo ambacho kingefanya tuiache ile barabara tuliyokuwa tunakuja nayo.

Jengo moja lenye ghorofa tatu lililojengwa vyema likiwa na rangi ya manjano, lilikuwa upande wa barabara ya pili kulia kwetu. Kulikuwa kimya. Nje ya ghorofa hilo taa zilikuwa zimewashwa kila upande wa jengo, huku wadudu aina ya kumbikumbi wakirukaruka juu yake. Ishara kuwa kilikuwa kipindi cha mvua. Hapakuwa na mtu pale nje.




"Mbele tena kwa upande wa ile barabara, kulikuwa na jengo jengine lenye ghorofa nne likiwa limepakwa rangi nyeupe."

Mbele tena kwa upande wa ile barabara, kulikuwa na jengo jengine lenye ghorofa nne likiwa limepakwa rangi nyeupe. Chini ya jengo hili palikuwa na fremu tano za maduka yaliyokuwa yamefungwa kwa wakati huo. Iliniwia vigumu kufahamu ni bidhaa gani zilikuwa zikiuzwa mchana kwenye zile fremu, lakini palionekana kuwa ni pahala penye biashara nzuri.

Watu watatu waliokuwepo nje ya lile jengo kwa pale chini walinifanya nisisimkwe mwili kutokana na namna ambavyo walikuwa wamekaa kuikabili hali ya ubaridi iliyokuwa ikitaradadi wakati ule.

Ilinibidi kufungua kioo cha dirisha la gari upande wangu na kutoa mkono kwa nje kupima hali ile kama vile afanyavyo mtu anayetaka kuoga maji ya moto anavyopima ukali wake na kisha kuchanganya na maji baridi mpaka yafikie kiwango anachokitaka. Wawili kati ya niliyowaona wamejibanza kwenye moja ya viambaza vilivyoko pale, walijifunika makoti mazito huku wamelalia maboksi.

Mwengine ambaye niliweza kumuona vizuri alikuwa amekaa kwenye kiti, alikuwa amevalia gwanda za rangi ya buluu ameshikilia rungu kwa mkono wake wa kulia. Nilipokaza macho vizuri na kumtazama niligundua kuwa ni mwanamke. Tena bila shaka ndiye mlinzi wa pale.

Aliinua uso wake haraka wakati mwanga wa teksi ulipommulika na kupita kama kishada, huku nikifunga kioo nilichokuwa nimekifungua. Gari ilikata kona na kufanya jengo hilo lililokuwa mbele yetu tulitazame kwa upande wa kulia. Dereva aliendelea kukanyaga mafuta na kuliweka gari sawa baada ya kuyumba kidogo kutokana na ukali wa ile kona. Niliteteka kidogo na kumtaza yule dereva alivyokuwa akiminyana, halafu nikageuza shingo nyuma kumtazama yule mwanamke mlinzi huku gari ikizidi kuyoyoma.

Kwa mbali sana kupitia kioo cha nyuma, nilimuona amesimama na kujinyoosha kidogo kisha akakaa tena pale kwenye kiti chake na kujiinamia.

"Maisha magumu kaka," alisema yule dereva wa teksi baada ya kugundua namtazama sana yule mwanamke.

Sikumjibu!

"Heri yake ameamua kufanya kazi, haibi cha mtu maskini ya Mungu na wala hafanyi umalaya; tofauti na madada zetu wengine ambao wanaona aibu kufanya kazi kama zile", aliongeza tena yule dereva kwa lafudhi yake ya ki-Tanga huku akijichekesha, kama kwamba niunge mkono kile alichokuwa anasema. Kama alivyotarajia nikajaa mzima mzima.

"Ni kweli usemalo kamanda, Mungu atamsaidia." Nilimjibu huku nikigeuka kutazama mbele. "Tena si ajabu ana familia inamtegemea" Niliongeza wakati najiweka sawa.

"Alaaah! Hilo mbona sio jambo la kuuliza, tena inawezekana anatoa mchango mkubwa sana katika familia yake" Alisema yule dereva huku akigeuka mara kadhaa na kunitazama.

"Lakini yule dada anaonekana bado ni mrembo, ina maana kakosa kweli mtu wa kumuweka ndani?" Nilimuuliza yule dereva baada ya kuwaza kwa nukta kadhaa.

"Mmh! Sina hakika na hilo, ila inategemea. Unajua maisha sasa hivi yamebadilika sana, uzuri umekuwa sio *ishu* tena, utatumia uzuri wako leo, kesho je? uzuri ukichuja utafanya nini hapo kaka? Kwa hiyo wanawake wameshtuka, wanajishughulisha na wao!" aliongea akinitazama tena. Akagundua namtolea macho.

"Vipi brother!" Akahamaki.

"Ukiongea tazama tu mbele nakusikia, ni hatari unachofanya"

"Aaah usijali, tushakuwa wazoefu sisi, mwaka wa 14 huu kwenye kazi hii na barabara zote hizi nazijua. Kuwa na amani *brother*" Alisisitiza.

"Siwezi kuwa na amani wakati miiko yako ya kazi unaikiuka!"

“Lakini *brother*….!”

“Hakuna cha lakini, tazama mbele!” Niliamrisha.

Nikamuona ametishika. Akatazama mbele na kuendelea na safari. Ukimya ukatawala kwa muda.

“Nasikia mabinti wa ki-Tanga sio mchezo kaka” Nilimsemesha kwa lengo la kumrudisha katika hali yake ya kawaida. Niliona akitabasamu kidogo. Akataka kunitazama, akajizuia.

“Aahh unauliza jembe shamba, huku unapokwenda ndio usiseme, utashindwa kujua uondoke na yupi. Siku hizi sio waja leo waondoka leo. Ni waja leo kuondoka majaaliwa!” Sote tukaangua kicheko mle garini, akaniletea mkono nigonge tano, nikampa!

Toka hapo akakata kona tena na kuingia barabara nyengine. Nikagundua ile barabara tuliyoingia awali haikuwa ndefu sana. Baada ya mwendo wa kama dakika moja na nusu akaiweka gari pembeni upande wa kushoto na kufunga breki.

“Tumefika mtu wangu” alisema yule dereva ambaye alijitambulisha kwa jina moja tu la Shehoza. “Ni pale mkuu” safari hii akionyesha kwa kidole upande wa pili kwenye jengo moja lililokuwa na maandishi makubwa yaliyowaka kwa taa ya rangi nyekundu kwa juu yaliyosomeka Sachakah House. Nililitazama lile jengo kwa makini kisha nikamgeukia Shehoza.

“Kiasi gani..?”

“Itakuwa elfu sita pamoja na ile ya kukusubiri pale Tanga Hoteli”.

Nikatoa pochi yangu ya pesa kwenye mfuko wa nyuma wa suruali na kumpatia noti ya shilingi elfu kumi.

“Unalala saa ngapi wewe, huwezi kunifuata wakati natoka?”

Wakati naongea yeye alikuwa akihangaika kutafuta chenji, na mimi nilikuwa naweka pochi yangu kwenye mfuko wa nyuma ilipokuwepo.

“Siku kama ya leo huwa silali mkuu, chukua namba yangu ya simu, ukitoka nipigie nitakufuata tu haina shida” alisema Shehoza.

Haraka nikatoa simu yangu na kuihifadhi namba yake aliyokuwa anaitaja. Nikaipiga na kisha simu yake ikaita.

“Ndio hii inayoita eenh” akaitoa simu yake iliyokuwa kwenye mfuko wa Shati alilokuwa amevaa. Akanipa chenji yangu, lakini sikumjibu kama alivyouliza, nilimwambia yangu inaishia na namba kumi mwishoni.

“Eee ndio yenyewe mkuu, basi poa. Ukitoka wewe nishtue halafu nitakufuata. Kwani si nakurudisha pale pale Silvarado Hoteli..?”

“Ndio”

Tukaagana.

* * *

Nilipoteremka kutoka mle garini cha kwanza nikasimama pembeni mwa barabara kwa lengo la kutathmini hali ya pale nje, watoto wa mjini wanasema *tunasoma ramani*. Ile teksi ikaondoka nikiwa nimesimama pale, nikaisindikiza kwa macho mpaka ilipotokomea.

Nilipoona hali ya pale nje ipo shwari nikavuka barabara na kuliendea lile jengo alilonionyesha yule dereva. Kulikuwa na baridi kiasi pamoja na upepo hafifu. Nilipotazama juu hakukuwa na nyota wala mwezi. Wingu lilikuwa limetanda.

Nje ya lile jengo hapakuwa pamechangamka sana japokuwa palikuwepo na watu wachache ambao baadhi yao walikuwa wamevalia nadhifu na kuonekana kutaka kuingia mle ndani. Akina dada wanne shombeshombe ambao walivalia *ki'disko disko* pamoja na wanaume watatu wenye asili ya kiarabu ambao nao pia walitoka *chicha* walikuwa wamesimama karibu kabisa na mlango wa kuingilia.

Wengine waliokuwepo pale ni walinzi wawili wa kiume ambao niliwatambua kwa mavazi yao pamoja na vijana wengine wawili. Hawa walikuwa wamejiegemeza ukutani huku wakitafuna kitu kama mirungi, maana midomo yao ilikuwa haitulii.

Karibu kabisa na hawa vijana palikuwepo pia na mchuuzi mmoja wa sigara, pipi, maji na bidhaa nyengine. Alikuwa amesimama akiwahudumia wateja zake.

Magari tofautitofauti ya kisasa yalikuwa yamejipanga kwa mstari yakiwa yamesogeleana karibu kabisa utadhani askari wa jeshi wanaofanya gwaride. Bila shaka aliyekuwa anawaelekeza namna ya kupaki alikuwa anaijua kazi yake vyema!

Kwa mwendo wa wastani nikawapita wale watu waliosimama pale karibu na pa kuingilia kama kwamba nilikuwa mwenyeji.

Wakati napita, dada mmoja kati ya wale wanne ambaye nilimshtukia akinitazama toka navuka barabara aligeuka na kunisindikiza kwa jicho kali sana. Alifanikiwa kuutetemesha moyo wangu, *Nilijali!* ...maana lile jicho halikuwa la kawaida. Nilitaka kugeuka lakini nilisita, nilihofia kumtazama kungeleta shida kwani nilihisi miongoni mwa wale vijana watatu pengine mmoja huenda akawa mwanaume wake. Nikampotezea!

Hata hivyo kwa haraka tu niliona amevaa blauzi nyekundu na jinzi ya rangi nyeusi. Nywele zake ndefu kama walivyo wanawake wa Brazili zilimfika mpaka mgongoni na kufanya aonekane kama mwanasesere. Alikuwa mweupe. Pamoja na kwamba nilikuwa nikimtazama kwa kuibia kwa mbali, lakini uzuri wake ulipiga kelele. Kwa mbali nikasikia harufu manukato makali.

"Wow…!" Neno hili lilinitoka tu. Sijui kama alinisikia, lakini nikahisi akizidi kunitazama, pengine aligundua ananitetemesha hivyo akataka sifa kunikodolea macho zaidi. Nilisimama baada ya kuona kibao kilichoandikwa *Club Lacasa Chica ghorofa ya pili*, nilipotazama upande wangu wa kushoto kulikuwa na ngazi. Sikutazama nyuma. Haraka kwa ushapu wangu uliochanganyika na ujanja wa mjini pamoja na muonekano wa kisasa nikaanza kuzisogelea zile ngazi.

Siku zote ni ngumu kumtambua mtu asili yake na mahala anapotoka hasa katika maeneo ya starehe kama haya ambayo hukutanisha watu tofauti tofauti. Labda awe Mmasai ambao mpaka leo wanasifika kwa kudumisha mila, tena awe na lubega yake huku ameshikilia sime pamoja na rungu ndio utamtambua, kama hana vitu hivyo basi utaaambulia patupu kumjua!

Nilipokuwa kwenye harakati za kutaka kupanda zile ngazi, nilishikwa na shauku kubwa kwa kuwa najua sasa lengo langu linakwenda kutimia kwani mpango wangu kuja kutembea Tanga ni kuonja uhalisia wa mapenzi ya wanawake wa ki-Tanga na urahisi wa kuwapata ni hapa klabu kwa kuwa taarifa nilishaipata toka nipo Arusha kwa rafiki yangu Maliki.

Niliambiwa zipo klabu nyengine, lakini hii ilikuwa ni zaidi ya zote. Kwani hata Ma'dj wake, mbali na kuwa na ujuzi mkubwa wa kuchanganya midundo ya nyimbo vizuri, lakini pia wanafanya kazi kwenye redio stesheni maarufu hapa jijini Tanga, hivyo wanatwanga ngoma kisawasawa.

Hiyo ndio sababu ya watu wengi kupapenda. Na siku ya Jumamosi kama ya leo huwa ni *ladies free* hivyo wanawake huwa wanajaa kuliko wanaume. Hapa ndipo nitakapopata kile nilichokifuata.

Kimoyomoyo nikasema, *patachimbika leo!*

# SURA YA PILI

Mara nikaipata tena ile harufu ya manukato niliyoisikia muda mchache uliopita, nikageuka kutazama nyuma. Duh! Alikuwa yule dada aliyekuwa akinitazama. Safari hii macho yake yaligongana na yangu kitendo kilichofanya nigeuke haraka na kuanza kuchapa lapa kupanda zile ngazi. Macho yake yalikuwa makali sana huku yamebeba kope ndefu zilizopakwa wanja. Kwa mara ya pili nikahisi mapigo yangu ya moyo yakitetereka.

***PAKUA KITABU KWA MUENDELEZO ZAIDI AU WASILIANA NA MWANDISHI KWA NAMBA 0719000010…***